WIZARA YA NISHATI

# News Bulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 63 | Machi 1 - 31 2025



# DKT.MWINYI AZIHAMASISHA NCHI ZA EAC KUANZISHA MIFUKO YA MAENDELEO YA PETROLI

WIZARA YA NISHATI +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**

Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika

**WAPIGA PICHA**

Henry Kilasila
Godfrey Mwemz
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo
Mustafa Shahame

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga


© NISHATI 2025

# DKT.MWINYI AZIHAMASISHA NCHI ZA EAC KUANZISHA MIFUKO YA MAENDELEO YA PETROLI

- Asema lengo ni kuwa na uhakika wa kuendeleza Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia
- Afunga Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Afrika Mashariki
- Ataka Rasilimali na Mafuta na Gesi Asilia kuchangia maendeleo ya Sekta nyingine



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi akizungumza wakati akifunga Kongamano na Maonesho ya Petroli Afrika Mashariki (EAPCE'25) ambalo limefanyika kwa Siku tatu jijini Dar es Salaam.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi amezihamasisha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na Mifuko ya Maendeleo ya Petroli (Petroleum Fund) ambayo itasaidia katika utafiti, ubunifu, mafunzo na uendelezaji wa Sekta ya Mafuta kwa ujumla.

Dkt. Mwinyi ameyasema hayo tarehe 07 Machi 2025 jijini Dar es Salaam wakati akifunga Kongamano na Maonesho ya Petroli Afrika Mashariki (EAPCE'25) ambalo limefanyika kwa Siku Tatu.

Ameeleza kuwa, Dira ya Afrika Mashariki ya 2050 inaelekeza kuhusu kuanzishwa kwa Mfuko huo wa Petroli hivyo huu ni wakati muafaka wa kutekeleza suala hilo kama lilivyoainishwa katika Ibara ya 114 ya Mkataba wa Afrika Mashariki ambayo inaelekeza kuimarisha mashirikiano katika kusimamia rasilimali kwa faida ya wote.

"Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaweza kujifunza kutoka kwa Umoja wa Wazalishaji wa Mafuta Afrika (APPO) kwa kushirikiana na Benki ya Afrexim ambao wamekubaliana kuanzisha Benki ya Nishati ya Afrika (AEB) ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika ufadhili ya miradi ya mafuta na gesi kwa kigezo cha kuchangia katika mabadiliko ya tabia nchi." Amesema Dkt.Mwinyi

Rais Mwinyi pia ameeleza kuhusu umuhimu wa Rasimali za Mafuta na Gesi Asilia kuwa na mchango katika ukuaji wa Sekta nyinginezo akitolea mfano jinsi Sekta ya Mafuta nchini ilivyosaidia miradi ya umeme hasa usambazaji wa umeme vijijini.

Aidha, amempongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kujitolea kwake bila kuchoka katika maendeleo ya sekta zote ikiwemo mafuta na gesi ambapo chini ya uongozi wake miradi ya kimkakati katika Sekta hiyo imeendelea kutekelezwa.

Pia, amezipongeza Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kufanya mkutano huo kwa mafanikio ikiwemo Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati ya kitaifa ya EAPCE 2025, Timu ya Kitaifa ya Uratibu na kamati zake ndogo.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt. Doto Biteko amesema kuwa. Mkutano huo uliofanyika kwa siku tatu umehusisha majadiliano, kubadilishana mawazo, kuwasilisha mawasilisho kutoka kwa Wataalam wa Sekta ya Mafuta na Gesi na kuangazia namna bora kutumia rasilimali za mafuta kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa uhakika, nafuu na usalama wa nishati.

Amesema Kongamano la EAPCE'25 limehudhuriwa na washriki zaidi ya 1400 kutoka nchi 25 na huo ukiwa ni ushuhuda wa dhamira ya dhati ya nchi wanachama wa EAC kukuza ajenda ya nishati ya uhakika kwa maendeleo endelevu ya watu.

# DKT. MPANGO ATAKA AFRIKA KUBUNI NJIA BORA UENDELEZAJI RASILIMALI ZA NISHATI KUKIDHI MAHITAJI

- Afungua Kongamano na Maonesho ya Petroli Afrika Mashariki (EAPCE'25)
- Asema upatikanaji wa Nishati Afrika bado ni mdogo kulinganisha na Mabara mengine
- Asisitiza uendelezaji wa vyanzo vya Nishati uzingatie mustakabali wa vizazi vijavyo




Makamu wa Rais, Mhe.Dkt. Philip Isdor Mpango, akizungumza wakati akifungua rasmi Kongamano na Maonesho ya Petroli Afrika Mashariki (EAPCE'25) ambalo limefanyika kwa Siku Tatu jijini Dar es Salaam.

Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango amesema kuna umuhimu Bara la Afrika hususan Kusini mwa Jangwa la Sahara kubuni njia bora za kuzitumia rasilimali zilizopo ikiwemo Mafuta na Gesi Asilia ili kuwawezesha wananchi kustawi kiuchumi na kijamii.

Amesema kuwa matumizi ya nishati Barani Afrika bado ni madogo ikilinganishwa na mabara mengine kama Amerika, Asia na Ulaya

Amesema hayo tarehe 5 Machi, 2025 wakati akifungua rasmi Kongamano na Maonesho ya Petroli Afrika Mashariki (EAPCE'25) ambalo lmefanyika kwa Siku Tatu jijini Dar es Salaam.

"Katika kipindi ambacho maendeleo ya nishati endelevu yana mchango mkubwa katika mustakabali wa mazingira, uchumi na jamii zetu na katika kipindi ambacho Dunia inakabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi bado tunahitaji kutumia rasilimali zetu zilizopo, ikiwemo mafuta na gesi asilia lakini bila kuhatarisha mustakabali wa vizazi vijavyo ili kukidhi mahitaji ya kinishati." Amesema Dkt. Mpango

Ameeleza kuwa, Afrika Mashariki imebarikiwa na rasilimali nyingi za nishati, ikiwemo mafuta na gesi asilia ambapo Tanzania imegundua gesi asilia, Uganda, Kenya na Sudan Kusini wamegundua mafuta, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo wana gesi ya methane, huku Kenya na Tanzania zikiwa na rasilimali za



nishati jotoardhi hivyo rasilimali hizo lazima zitumike ili kupunguza pengo la nishati na kuharakisha maendeleo.

"Tunatambua kuwa ulimwengu unakabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha madhara makubwa kama vile vipindi visivyotabirika vya mvua, mafuriko, mitetemeko ya ardhi na kuongezeka kwa joto. Tanzania, kama mataifa mengine, imejitolea kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kufanikisha azma ya kutozalisha hewa ya kaboni ifikapo mwaka 2050. Hata hivyo, tunapaswa kuweka uwiano kati ya ukuaji wa uchumi na uendelevu wa vyanzo vyetu kwa kutatua changamoto za leo huku tukijiandaa kwa changamoto za kesho." Amesema Dkt. Mpango

Dkt. Mpango ameeleza kuwa, suala la kuhama kutoka kwenye nishati chafu kwenda kwenye nishati safi haliepukiki kwani ni mkakati muhimu wa kupunguza uchafuzi wa mazingira duniani hata hivyo uwekezaji katika nishati hiyo unahitaji mtaji mkubwa na utaalamu wa hali ya juu ambapo inakadiriwa kuwa Afrika inahitaji kati ya Dola Trilioni 1 hadi 2 kufanikisha malengo ya ya kuelekea kwenye nishati safi ifikapo mwaka 2030 hivyo kuna umuhimu wa kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji na kuwa na ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma.

Katika Mkutano huo wa EAPCE'25, Dkt, Mpango amesema kuwa anaamini Viongozi na Wataalam watabadilishana mawazo na uzoefu kuhusu kufungua fursa za uwekezaji katika nishati endelevu bila kusahau nafasi ya rasilimali za mafuta katika upatikanaji wa nishati ya kutosha huku akisisitiza ushirikiano wa kikanda kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa, kadri uchumi unavyokua kwa kasi mahitaji ya nishati hasa Gesi Asilia yanaongezeka hivyo Serikali inaendelea na jitihada za kuendeleza miradi ya mkondo wa juu wa petroli kwa lengo la kugundua na kuendeleza vyanzo vipya vya rasilimali za Mafuta na Gesi Asilia.

" Nampongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuendeleza mkondo wa juu wa petroli ambapo chini ya uongozi wake uzalishaji wa gesi umeimarika katika vitalu vya Songosongo na MnaziBay ambavyo ni muhimu katika uchumi wa gesi."Amesema Dkt.Biteko

Dkt.Biteko ametaja baadhi ya mafanikio katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia nchini kuwa ni pamoja na uendelezaji wa gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la Ntorya kitalu cha Ruvuma kwa kutoa leseni uendelezaji wake kwa kampuni ya ARA Petroleum na kuongezeka kwa ushiriki wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika kitalu cha Mnazibay kutoka asilimia 20 hadi 40.

Naye Waziri wa Nishati wa Uganda, Mhe. Ruth Nankwabira ameeleza kuhusu umuhimu wa fedha zinazopatikana katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kunufaisha Sekta nyingine huku akitolea mfano kuwa nchini Uganda wameanzisha Mfuko wa Petroli ambao unahudumia sekta nyingine ikiwemo barabara, elimu, afya lengo likiwa ni kuhakikisha kila mtu anafaidika na sekta husika.
Amesema sekta ya Mafuta na Gesi ni muhimu katika kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia hali itakayowezesha pia kupunguza uharibifu na misitu ambapo amempongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa Nishati Safi ya Kupikia Duniani.

Katibu Mtendaji Jumuiya ya Afrika MasharikiVeronica Nduva, amepongeza Tanzania kuendesha mkutano huo kwa mafanikio na kueleza kuwa unaendana na malengo ya Jumuiya ya EAC ya kuhakikisha kunakuwa na uendelezaji wa rasilimali za Mafuta na Gesi Asilia unaozingatia utunzaji wa mazingira.

# AFRIKA TUNAYAPA KIPAUMBLE MATUMIZI YA NISHATI SAFI ILI KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI-DKT. BITEKO

- Asema Sera na Sheria zinazowekwa zinahimiza matumizi ya Nishati Safi
- Afungua Mkutano wa Awali EAPCE'25
- Ataka utumike kujadili na kuweka mipango itakayowezesha matumizi ya Nishati Safi
- Ataka mkazo kuwekwa kwenye Nishati Safi ya Kupikia kwani matumizi ya kuni na mkaa bado ni makubwa




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt.Doto Biteko akifungua Mkutano wa awali kuelekea Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) litakaloanza rasmi kesho jijini Dar es Salaam ambapo mkutano huo wa awali ulilenga kujadili mipango na mikakati itakayopelekea matumizi ya nishati safi katika maeneo mbalimbali ikiwemo kupikia na vyombo vya usafiri (CNG).

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema licha Bara la Afrika kuwa na mchango mdogo katika uchafuzi wa hali ya hewa, nchi za Afrika bado zimekuwa mstari wa mbele katika kuendesha ajenda ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuijumuisha katika mifumo yao ya kisheria na udhibiti ikiwemo ya kuhakikisha kuwa nchi zinahama kutoka kwenye matumizi ya nishati chafu na kutumia nishati safi ili kuiepusha dunia na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Dkt. Biteko amesema hayo tarehe 4 Machi, 2025 jijini Dar es Salaam wakati akifungua Mkutano wa awali kuelekea Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) litakaloanza rasmi kesho ambapo mkutano huo wa awali ulilenga kujadili mipango na mikakati itakayopelekea matumizi ya nishati safi katika maeneo mbalimbali ikiwemo kupikia na vyombo vya usafiri (CNG).

Amesema mkutano wa EAPCE' 25 ni jukwaa muhimu kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wadau wengine kujadili mipango na mikakati kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt.Doto Biteko (katikati) akiimba Wimbo wa Taifa wakati wa Mkutano wa awali kuelekea Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) litakaloanza rasmi kesho jijini Dar es Salaam ambapo mkutano huo wa awali ulilenga kujadili mipango na mikakati itakayopelekea matumizi ya nishati safi katika maeneo mbalimbali ikiwemo kupikia na vyombo vya usafiri (CNG). Kulia kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga na kushoto kwake ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

hasa ikizingatiwa kwa sasa dunia inapambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na shughuli za binadamu huku tafiti za kisayansi zikionesha kuwa viwango vya utoaji wa hewa ya ukaa vimeongezeka kwa kiasi kikubwa tangu kufanyika kwa Mapinduzi ya Viwanda.

"Nataka nichukue nafasi hii kuwaomba wote muutumie mkutano huu kujadili masuala ambayo yatatufanya sisi wana Afrika Mashariki, tuweze kuhama kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyokuwa safi kwenda kwenye matumizi ya nishati iliyosafi, lazima mtambue kwamba mkutano huu wa awali haujatokea kwa bahati mbaya, kama jamii tunayo kazi ya kufanya ya kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyo safi kwenda matumizi ya nishati safi." Amesisitiza Dkt.Biteko

Ameeleza kuwa, sheria nyingi zinazopitishwa kwa sasa barani Afrika zinahimiza uchumi wa kijani, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuwa na maendeleo endelevu ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa upande wake imeandaa Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni uthibitisho wa dhamira ya kanda hiyo katika kushughulikia tatizo la mabadiliko ya tabia nchi na kuhimiza matumizi ya nishati safi.

Ametaja baadhi ya athari za mabadiliko ya tabia nchi kuwa ni pamoja na ukame mkali, mafuriko, kupotea kwa viumbe hai, kupungua kwa vyanzo vya maji safi, kuyeyuka kwa barafu, na ongezeko la magonjwa yanayohusiana na tabianchi kama vile saratani ya ngozi.

Dkt.Biteko ameeleza kuwa suala la mabadiliko ya tabia nchi linatiliwa mkazo pia katika ngazi ya dunia na hii imepelekea kuwepo kwa mikataba mbalimbali ya kimataifa ukiwemo wa Kyoto, Montreal na Paris ambapo nchi zilizoendelea na zinazoendelea zinaandaa na kutekeleza mikakati inayohusiana na tabianchi ikiwemo kujikita katika matumizi ya nishati safi zisizochafua mazingira ikiwemo Gesi Asilia.

Kuhusu upatikanaji umeme amesema Afrika ndiyo Bara inalokabiliwa na upungufu mkubwa wa nishati duniani, ambapo asilimia 75 ya watu wanaokosa nishati duniani wanapatikana barani humo lakini juhudi zinafanyika ili kuwezesha upatikanaji wa nishati na hili lilithibitishwa kupitia Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati uliofanyika Tanzania Januari mwaka huu ambao uliweka mikakati ya kuongeza upatikanaji wa umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo mwaka 2030 ambayo ni hatua muhimu kuelekea mabadiliko ya kinishati.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia amesema mabadiliko yanahitajika ili kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi kwani idadi kubwa ya watu barani Afrika bado wanategemea kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia akitolea mfano nchini

Tanzania, takriban asilimia 81 ya kaya zinatumia kuni na mkaa kama vyanzo vyao vikuu vya nishati ya kupikia, hali inayosababisha upotevu wa misitu wa takriban hekta 469,420 kila
mwaka akitanabaisha kuwa mwelekeo huo wa kutisha unahitaji hatua za haraka na za pamoja ili kuendeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia barani kote.

Amesema katika kukabiliana na changamoto hiyo nchini Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,
ambaye ni kinara wa ajenda nishati safi ya kupikia kitaifa na
kimataifa kwa ujumla amechukua hatua madhubuti kwa kutekeleza Mkakati wa Kitaifa Nishati Safi ya Kupikia (2024–2034) ambao unalenga kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Aidha amesema kuwa, matumizi ya gesi asilia kama nishati ya kuendeshea vyombo vya usafiri pia ni muhimu katika kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi akieleza kuwa Serikali ya Tanzania inaendelea kuboresha mazingira kwa wawekezaji binafsi kushiriki katika ujenzi wa Vituo vya Gesi Asilia Iliyoshindiliwa (CNG) na kuboresha sera na mifumo ya udhibiti.

Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga kwa upande wake amesema mkutano huo wa awali unaweka msingi wa Kongamano la 11 la Mafuta kwa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki litakaloanza kesho Machi 05, 2025.

"Siku ya leo kutakuwa na mada mbalimbali zitakazozungumzwa, ambazo zitakuwa na majadiliano yatakayoweka msingi kwa ajili ya mkutano mkuu utakaoanza kesho na kufanyika kwa siku tatu, mkutano huu ni muhimu katika kuwaweka wadau pamoja na kujadiliana masuala ya msingi ambayo yatazisaidia Nchi za jumuia ya Afrika Mashariki katika Sekta ya Mafuta na Gesi." Amesema Kapinga

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema kuwa mkutano huo wa Mafuta na Gesi unaenda sambamba na Maonesho ya bidhaa za mafuta na gesi pamoja na kazi mbalimbali zinazofanyika katika sekta miongoni mwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika
Mashariki.

Ameeleza kuwa, Mkutano umelenga kuangalia namna bora ya kuhama kutoka kwenye nishati zinazochafua mazingira kwenda kwenye nishati safi zisizochafua mazingira ikiwa ni kampeni ya dunia ambayo imetokana na
malengo ya dunia ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2050 hadi 2060 dunia iwe imeweza kuhamia kwenye nishati safi kwa kiasi kikubwa.

Mhandisi Mramba ameeleza kuwa, katika mkutano huo nchi zitapata nafasi ya kuelezea maendeleo waliyofanya katika eneo la mafuta na gesi ambapo Makatibu Wakuu na Mawaziri watazungumza kuhusu mafanikio,
mipango na kazi zilizofanyika tangu kufanyika kwa mkutano uliopita wa
EAPCE.

Amesema katika mkutano wa EAPCE'25 wataalam, watafiti na wabunifu mbalimbali watazungumzia ugunduzi wa mafuta na gesi, sehemu ambazo vitalu vinanadiwa na kukaribisha uwekezaji kwa nchi za EAC.





# SEforALL KUIMARISHA USHIRIKIANO UPATIKANAJI NISHATI ENDELEVU

- Dkt. Biteko asema Nishati Safi ya Kupikia ni ajenda endelevu
- Rais wa Sierra Leone asema ukombozi wa maeneo ya vijijini ni muhimu kufikia maendeleo
- Waziri Mkuu wa Barbados apendekeza ushirikiano wa kimataifa kumaliza changamoto za nishati




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza katika mkutano wa kimataifa kuhusu matumizi ya nishati endelevu kwa watu wote uliofanyika nchini Barbados.

Viongozi mbalimbali wanaoshiriki mkutano wa kimataifa kuhusu matumizi ya nishati endelevu kwa watu wote unaofanyika nchini Barbados wameshauri kuimarishwa kwa ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuwezesha upatikanaji wa nishati endelevu kwa gharama nafuu.

Akizungumza katika mkutano huo unaofanyika jijini Bridgetown, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema Tanzania kwa upande wake chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imepanga kuwawezesha asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Amesema, kupitia mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) unaozalisha megawati 2,115 utawezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika na endelevu kwa maendeleo na ustawi wa wananchi katika ngazi mbalimbali.

Dkt. Biteko amesisitiza kuwa, utekelezaji wa lengo namba 7 katika mpango wa maendeleo ya milenia unahitaji ushirikiano miongoni mwa Serikali na sekta binafsi katika kuboresha upatikanaji wa nishati safi ikiwa ni moja ya utatuzi wa changamoto zilizopo.

Amesema ni muhimu kwa mataifa kuwekeza katika miundombinu kwa ajili ya upatikanaji wa nishati safi sambamba na kuweka mifumo ya ubunifu na utashi katika kuwezesha upatikanaji wa nishati kwa usawa bila kuacha makundi mengine.

Naye, Waziri Mkuu wa Barbados, Mhe. Mia Mottley amesema ni

wakati sasa wa kuweka mkakati wa kimataifa na kukubaliana kushirikiana kumaliza changamoto ya upatikanaji wa nishati kwa wote.

Akizungumzia mkutano wa misheni 300 (M300) uliofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Waziri Mkuu Mia amesema inatia simanzi kuwa na watu zaidi ya milioni 600 barani Afrika wanaishi bila huduma ya umeme suala ambalo limesababisha changamoto katika nchi nyingi duniani.

"Tunahitaji kupata ufumbuzi wa changamoto zilizopo, uwe ufumbuzi wa ndani au kutoka katika nchi yoyote duniani," amesema Mhe. Mottley.

Kwa upande wake, Rais wa Sierra Leone, Mhe. Julius Maada Bio amesema katika kipindi hiki ambapo nishati ni nyenzo muhimu katika upatikanaji wa maendeleo, ni muhimu kuwezesha watu na makundi yote kupata nishati hususani katika maeneo ya vijijini yanayokabiliwa na umasikini uliokithiri.

"Wanawake na watoto ambao wanatumia muda mwingi kutafuta nishati ambayo sio safi kwa ajili ya kupikia, wanatakiwa kuwezeshwa kupata nishati safi na hivyo kutumia muda mwingi kufanya shughuli za maendeleo," ameongeza.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Mtendaji Mkuu SEforALL, Damilola Ogumbiyi, amesema zinahitajika ajenda madhubuti za kuwezesha kukabiliana na vitendo vinavyotokana na matumizi ya nishati isiyo safi

"Tumeshuhudia matokeo yanayosababishwa na ukosefu wa nishati safi kama vile uharibifu wa mazingira unaosababisha ukame na mafuriko ambayo kwa kupata nishati safi tunaweza kuondokana nayo," amesema.

Mkutano huo wa kimataifa ni mwendelezo wa mikutano ya kikanda na kimataifa inayokusudia kupata suluhisho la changamoto zinazotokana na matumizi ya nishati chafu.

Mwezi Januari, 2025, viongozi na wakuu wa nchi mbalimbali barani Afrika na taasisi mbalimbali za fedha ikiwemo Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika walikutana jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kutafuta uwezekano wa kuwawezesha watu takribani milioni 300 barani Afrika kupata huduma ya nishati ya umeme.

# TANZANIA NA MISRI KUENDELEZA USHIRIKIANO KWENYE MIRADI YA UMEME -KAPINGA

- Waziri wa Mambo Nje Misri atembelea Bwawa la Julius Nyerere
- Asifu hatua za Rais wa Tanzania na Misri kusimamia utekelezaji wa mradi
- Mradi wafikia asilimia 99.89

Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga, amesema Tanzania na Misri zitaendeleza ushirikiano kwenye utekelezaji wa miradi ya umeme na kudunisha ushirikiano uliowekwa na waasisi wa nchi hizo.

Mhe Kapinga ameyasema hayo tarehe 20 Machi,2025, mkoani Pwani wakati alipofanya ziara katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje, Uhamiaji na Wamisri waishio nje ya Jamhuri ya Misri, Dkt Badir Abdelatty ikiwa ni sehemu ya ziara ya kikazi ya Waziri Badir na ujumbe wake.

''Tunamshukuru sana Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwani amekuw msingi imara wa utekelezaji wa miradi huu wa umeme na tumeona matunda halisi ya usimamizi wake." Amsema Mhe.Kapinga

Amesema nchi ya Misri imetekeleza mradi huo wa JNHPP kwa kuzingatia matakwa ya nchi ya Tanzania ambapo mpaka sasa mashine nane kati ya tisa zimewashwa na kuingizwa kwenye gridi ya Taifa

Akizungumza mara baada ya kutembelea na kujionea maendeleo ya mradi wa JNHPP, Waziri, Dkt Badir Abdelatty, amesifu ushirikiano wa muda mrefu uliopo kati ya Tanzania na Misri na kuishukuru Tanzania kwa kuiamini nchi yake kutekeleza mradi huo wa JNHPP,



kwani utawanufaisha wananchi wa Tanzania walio wengi hususani wale wanaozungukwa na eneo la mradi.

Amesema nchi za Afrika zinapaswa kujivunia uwepo wa miradi ya umeme kwa maendeleo ya waafrika wenyewe na kuahidi kuwa Misri itaendeleza ushirikiano na Tanzania kwenye utekelezaji wa miradi mingine kama hiyo

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Mambo ya Nje anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki Mhe Dannis Londo amesema, Tanzania na Misri zitaendeleza ushirikiano wa kidiplomasia ulionao ili kufungua fursa mbalimbali za kiuchumi hususani kwenye miradi ya sekta ya Nishati

Ziara hiyo.imehudhuriwa na Balozi wa Tanzania nchini Misri, Balozi wa Misri nchini Tanzania, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Mafuta, Dk James Mataragio, na viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga ( wan ne kushoto) akiwa katika kwenye mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje, Uhamiaji na Wamisri waishio nje ya Jamhuri ya Misri, Dkt Badir Abdelatty ( wan ne kulia) tarehe 20 Machi 2025. Wa tatu kulia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki Mhe Dannis Londo

# KAPINGA AZINDUA NAMBA YA BURE YA HUDUMA KWA WATEJA WA TANESCO

- Awapongeza TANESCO kutekeleza agizo la Mhe. Dkt. Biteko kuwataka kuanzisha namba ya huduma kwa wateja bure
- Asema namba hii ya 180 ya bure kwa wateja kuimarisha huduma kwa wateja na kutatua changamoto zao
- Awaagiza Mameneja wa Mikoa na wilaya wa TANESCO kuwasimamia watoa huduma
- Awaasa watanzania kutumia namba hiyo kwa malengo yaliyokusudiwa na si vinginevyo



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga akizungumza wakati wa uzinduzi wa namba mpya ya huduma kwa wateja (mchongo 180) itakayotumiwa na wateja bure bila malipo.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga Machi 12, 2025 amezindua namba mpya ya huduma kwa wateja (mchongo 180) itakayotumiwa na wateja bure bila malipo ili kupata huduma mbalimbali kupitia kituo cha miito ya simu cha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Kuanzishwa kwa namba hiyo inafuatia agizo lililotolewa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko la kuwataka TANESCO kuhakikisha wanakuwa na namba ya bure bila malipo kwa wateja ili kuboresha utoaji huduma kwa wateja na kupunguza malalamiko yasiyo ya lazima na kuongeza wigo wa wapokeaji wa simu kutoka namba ya awali hadi 150 kwa awamu.

''Naomba niwahakikishie kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imekusudia watanzania wapate umeme wa uhakika na kuongeza kuwa Wizara ya Nishati itaendelea kuisimamia TANESCO na taasisi nyingine chini ya Wizara kuhakikisha sekta ndogo ya umeme inakuwa na kuleta maendeleo kwa Watanzania.

Awali akizungumza kabla ya mgeni rasmi, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO, Balozi Zuhura Bundala amesema mapinduzi kwenye utoaji huduma kwa wateja ni moja ya masuala ya kipaumbele ili kuchochea uchumi wa Nchi na kuongeza kuwa shughuli za uchumi zinategemea sana uwepo wa umeme wa kutosha na uhakika na ndio maana bodi imejipanga kutekeleza maagizo mbalimbali yanayotolewa na Wizara.

Amesema bodi iko tayari kuhakikisha TANESCO inafanya kazi kwa bidii na jkutoa huduma bora kwa wateja ili kupunguza kero na changamoto za masuala mbalimbali.


Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mha. Gissima-Nyamo Hanga amesena dunia ya sasa ya biashara na ushibdani wa kibiashara unategemea uwepo wa huduma bora ya uneme na kutatua changamoto kwa wakati

Aidha, Mha. Gissima amesema licha ya kujipanga kutoa huduma bora kwa wateja pia wamekuwa wakitekeleza kwa vitendo uhamasishaji wa matumizi bora ya nishati kwa kutumia umeme.

Hafla hiyo imehudhuriwa na wawakilishi kutoka Wizara ya Nishati, bodi ya wakurugenzi ya TANESCO na wadau mbalimbali

# SERIKALI KUJENGA MTANDAO MKUBWA WA MABOMBA YA GESI-DKT.BITEKO

- Asema lengo ni kurahisisha huduma kwa wananchi
- Afanya mazungumzo na kampuni Rashal Energies inayojenga Bomba la Gesi Kisemvule-Mbagala
- Aikaribisha kampuni ya CNOOC kushiriki Duru ya Tano Vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwa katika picha ya pamoja na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Rashal Energies, Farhiya Warsame mara baada ya kumaliza mazungumzo jijini Dar es Salaam tarehe 06 Machi, 2025 kando ya Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) linalofanyika kwa Siku Tatu jijini Dar es Salaam.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amekutana na kufanya mazungumzo na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Rashal Energies, Farhiya Warsame ambayo inajenga Bomba la Gesi kutoka Kisemvule hadi Mbagala jijini Dar es Salaam kwa ajili ya matumizi ya vituo vya Kujazia Gesi kwenye Magari (CNG) na kwenye viwanda.

Mazungumzo hayo yamefanyika jijini Dar es Salaam tarehe 06 Machi, 2025 kando ya Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) linalofanyika kwa Siku Tatu jijini Dar es Salaam.

Dkt.Biteko amesema kuwa lengo la Serikali ni kuwa na mtandao mkubwa wa mabomba ya gesi pamoja na vituo vya kujazia gesi kwenye magari ili kuwawezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi.

Kutokana na hilo Dkt.Biteko ameeleza kuwa Serikali ipo tayari wakati wowote kutoa ushirikiano kwa kampuni zinazotaka kuwekeza kwenye kutoa huduma hiyo kwa wananchi.

Kwa upande wake, Bi.Farhiya Warsame amemshukuru Dkt. Biteko kwa miongozo yake ambayo imepelekea kampuni hiyo kuanza kutekeleza mradi huo.


Ameeleza kuwa wananchi wameonesha mwamko mkubwa kwenye kuendesha vyombo vyao vya usafiri kwa kutumia gesi asilia badala ya mafuta kutokana na gesi asilia kuwa na gharama nafuu kuliko mafuta.

Vilevile, Dkt. Biteko amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa kampuni ya Rock Mountain ya nchini Canada, Bw. Nick Lenstra ambayo imesaini Mkataba wa Ushirikiano na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa ajili ya kuanza kazi za upembuzi yakinifu na kuzungumza na wadau wa ndani ikiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) ili kutumia gesi asilia kutengeneza nishati kwa njia ya kimiminika ambayo inaweza kutumika kwenye ndege.

Hali kadhalika, Dkt.Biteko amekutana na kufanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa kampuni ya CNOOC kwa upande wa Uganda, Wang Juteng ambapo pamoja kuzungumzia Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia nchini, ameikaribisha kushiriki Duru ya Tano ya Kunadi Vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia nchini.

# DKT. SAMIA AMETENDA MAAJABU SEKTA YA NISHATI MIAKA MINNE YA UONGOZI- DKT. BITEKO

- Mashine ya 9 yakabidhiwa, yakamilisha MW 2115 -JNHPP
- Aitaka Jumuiya ya Wazazi ieleze Watanzania mafanikio ya Serikali
- Asema kuongezeka kwa mahitaji ya umeme nchini kunachochea ukuaji wa viwanda
- Atoa wito kwa Watanzania kuzingatia matumizi bora ya umeme




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwasilisha mada kuhusu ongezeko la mahitaji ya umeme nchini katika Kikao cha Baraza Kuu la Wazazi Taifa kilichofanyika leo Machi 23, 2025 jijini Arusha.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan sekta ya nishati imepiga hatua kubwa nchini sambamba na kuzalisha umeme wa ziada dhidi ya mahitaji ya Watanzania.

Dkt. Biteko amesema hayo Machi 23, 2025 jijini Arusha wakati akitoa takwimu kuhusu ongezeko la mahitaji ya umeme nchini katika Kikao cha Baraza Kuu la Wazazi Taifa.

" Rais Samia amefanya kazi kubwa katika sekta ya nishati nchini na hivi karibuni, tulikuwa nchini Barbados kueleza mafanikio yetu katika sekta hii kwa kuwa Rais Samia amefanya jitihada kubwa sana katika ya nishati," amesema Dkt. Biteko.

Ameongeza "Ili uchumi wa nchi yoyote duniani upatikane lazima kuwe na sekta ya nishati. Aidha, katika sekta ya nishati ili viwanda viweze kuendelea umeme unaohitajika ni asilimia 40 na katika sekta ya madini umeme unaohitajika ni asilimia 30,"

Dkt. Biteko amesema mwaka 2017 hadi 2018 mahitaji ya juu ya umeme nchini yalikuwa megawati 1045, mwaka 2018 hadi 2019 mahitaji ya juu ya umeme yalikuwa megawati 1,116 mwaka 2021 hadi 2022 megawati 1,340.7.

" Mwaka 2022 hadi 2023 mahitaji ya juu yaliyoongezeka na kufikia megawati 1,470 na mwaka 2024 hadi kufikia sasa mwaka 2025 ni megawati 1,908 ikiwa ni sawa na megawati 262, ongezeko la mahitaji ya namna hii haliwezi



Sehemu ya wajumbe wa Kikao cha Baraza Kuu la Wazazi Taifa wakimsikiliza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko wakati akiwasilisha mada kuhusu ongezeko la mahitaji ya umeme nchini katika Kikao cha Baraza Kuu la Wazazi Taifa kilichofanyika leo Machi 23, 2025 jijini Arusha.

kutokea kama hakuna uwekezaji katika sekta ya nishati," amesema Dkt. Biteko.

Amesisitiza kuwa kutokana na ongezeko hilo la megawati za umeme Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere pekee linaweza kutosheleza mahitaji ya nchi licha ya kumalizika kwa muda uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo ya Songas. Aidha, Machi 22, 2025 mashine ya tisa ya mtambo wa kuzalisha umeme katika Bwala la Julis Nyerere imewasili nchini.

"Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan sekta ya nishati imefanya kazi kubwa, Rais Samia ametenda maajabu katika sekta hii na ameweza kuvutia wawekezaji wengi sana kuja kuwekeza nchini," amesema Dkt. Biteko.

Aidha, amesema kuwa Jumuiya ya Wazazi nchini ina wajibu wa malezi na mazingira na kuwa nishati safi ni eneo mojawapo hivyo Wizara ya Nishati ina wajibu wa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Jumuiya hiyo, sambamba na kushirikiana nayo katika kampeni zake za kupeleka ujumbe kwa jamii.

Pamoja na hayo, Dkt. Biteko amewaasa Watanzania kuzingatia matumizi bora ya umeme kwa kuacha mazoea yanayosababisha upotevu wa umeme ikiwemo kuwashaa taa bila kuwa na matumizi nazo.

Ametolea mfano kuhusu matumizi mabaya ya umeme kupitia utafiti uliofanywa na Wakala wa Nishati wa Kimataifa (International Energy Agency) ambapo asilimia 30 ya umeme unapotea kutokana na mazoea.

Katika hatua nyingine, taasisi mbalimbali ikiwemo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) zimewasilisha mada mbalimbali katika semina hiyo.

Pia, Wizara ya Nishati kupitia taasisi zake za TPDC, REA na TANESCO zimetoa semina kwa wajumbe wa kikao hicho kuhusu Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2024 hadi 2034, Matumizi Sahihi ya Nishati Safi ya Umeme.

Ambapo, Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia, kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Ngeleja Mugejwa ameeleza faida mbalimbali za matumizi ya nishati safi ya kupikia hususan kwa watoto wa kike ambapo kupitia matumizi ya nishati hiyo itawasaidia kupata muda mwingi wa kujisomea kuliko kuandaa na kupika chakula.

# UMEME WA JOTOARDHI KUUNGANISHWA KWENYE GRIDI YA TAIFA IFIKAPO 2030 - MRAMBA

- Mikoa 16 kunufaika na Nishati ya Jotoardhi
- SEforALL yatakiwa kuwekeza katika utafiti na ubunifu



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba akizungumza katika mjadala wa viongozi wanaoshiriki mkutano wa Kimataifa wa nishati endelevu kwa wote (SEforALL) unaofanyika katika jiji la Bridgetown nchini Barbados.

Tanzania imelenga kuunganisha nishati ya jotoardhi kwenye gridi ya taifa ifikapo mwaka 2030 ili kuwa na umeme wa uhakika unaotokana na nishati jadidifu kuelekea Dira ya Tanzania 2025 ambayo inasisitiza maendeleo endelevu ya nishati kama nguzo ya mabadiliko ya kiuchumi.

Hayo yamebainishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba katika mjadala wa viongozi wanaoshiriki mkutano wa Kimataifa wa nishati endelevu kwa wote (SEforALL) unaofanyika katika jiji la Bridgetown nchini Barbados.

"Lengo letu ni kuunganisha nishati ya jotoardhi kwenye gridi ya taifa ifikapo 2030, Suala hili ni miongoni mwa azma yetu pana ya kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa wote ifikapo 2030 ili kuondokana na uzalishaji wa hewa ukaa ifikapo 2050. Hii ni kutokana na Sera ya Taifa ya Nishati ya Tanzania 2015 yenye Mpango Mkuu wa Nishati 2020 pamoja na Tamko la Dar es Salaam la "Mission 300" katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika wa 2025". amesema Mha. Mramba

Mha. Mramba amesema kuwa, mikoa 16 nchini Tanzania itanufaika na maendeleo ya nishati ya jotoardhi, na kuifanya kuwa msingi wa mkakati wa nishati endelevu, Nia hii inajidhihirisha kupitia uanzishwaji wa Kampuni ya Maendeleo ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) kwa lengo la kutafiti na kuendeleza rasilimali za jotoardhi ambapo hadi sasa kampuni hiyo inafanya kazi katika maeneo zaidi ya 50.

Aidha Mha. Mramba, amesema kuwa ili kuvutia uwekezaji, Serikali imeweka mfumo madhubuti wa Sera na udhibiti kuvutia wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali ili kufanya tafiti na kufungua uwezo kamili wa rasilimali hiyo kuwa chachu kwa taifa, "Kwa kutambua umuhimu wa kimkakati, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeipa kipaumbele nishati ya jotoardhi katika ajenda ya kitaifa ya maendeleo ya nishati".

Naye, Waziri wa Nishati wa Shirikisho la St. Kitts na Nevis, Mhe. Konris Maynard amesema kuwa nchi zinatakiwa ziwe tayari kukuza matumizi ya jotoardhi na kuhama katika katika matumizi ya nishati zisizo salama kwa mazingira. Aidha amewataka wadau walioshiriki mkutano huo kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati ya jotoardhi.

Tanzania imebarikiwa kuwa na uwezo mkubwa wa nishati ya jotoardhi, unaokadiriwa kuwa zaidi ya 5,000 MW za umeme na 15,000 MW za nishati ya joto. Vilevile, Tanzania ina bahati ya kuwa katika eneo la kijiografia ambapo kwa upande Mashariki na Magharibi imezungukwa na Bonde la Ufa la Afrika Mashariki (EARS), hali hii inaifanya Tanzania kuwa na msingi wa kijiolojia unaofaa kwa ajili ya kutumia rasilimali hiyo Jadidifu.

# DKT. BITEKO AWAPONGEZA WABUNGE KWA KUWASEMEA WATANZANIA

- Asema Serikali itaendelea kuwawezesha wazawa kushiriki miradi ya nishati
- Asema sekta ya nishati imepiga hatua kubwa

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewapongeza waheshimiwa wabunge kwa kuihimiza Serikali kuendelea kuwezesha wazawa kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya sekta ya nishati.

Dkt. Biteko amesema hayo Machi 24, 2025 wakati akijibu hoja za wabunge katika kikao cha Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini kuhusu randama ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/26 kilichofanyika bungeni Dodoma.

" Nakubaliana na wabunge kuhusu kuangalia wazawa na kuwapa nguvu ili waweze kushiriki katika miradi ya nishati, tumekuwa tukifanya hivyo lakini tutaendelea kuangalia wazawa wenye uwezo ili tufanye nao kazi. Ninawashukuru sana waheshimiwa wabunge kwa kuwasemea Watanzania ili washiriki katika miradi," amesema Dkt. Biteko



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akijibu hoja za wabunge katika kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu randama ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/26 kilichofanyika leo 24 Machi 2025

Ameongeza kuwa licha ya kuwa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Serikali itaangalia zaidi namna ya kusaidia wazawa katika sekta ya nishati, huku akitolea mfano hatua iliyopigwa katika sekta hiyo.

Amesema kuwa kwa sasa Serikali imeliwezesha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kuwa na uwezo kuzalisha na kusambaza umeme nchini kwa kuimarisha mifumo na miundombinu mbalimbali.

" Mwaka huu unaopita Watanzania 53,000 wamepata ajira katika sekta hii. Tumepokea pia maoni ya waheshimiwa wabunge kuhusu uwepo wa wazawa kwenye kila kampuni inayopewa kazi na kuangalia upya mfumo wa utoaji zabuni," amesema Dkt. Biteko.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko amesema kuwa mara baada ya kukamilisha mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, Serikali inaanzisha miradi mipya ya kuzalisha umeme kwa kuwa mahitaji ya juu ya umeme yamekuwa yakiongezeka hadi kufikia megawati 253 mwaka 2025.

Aidha, kupitia kikao hicho kilichoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Dkt. Mathayo David kimejadili kuhusu randama ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/26.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. David Mathayo David akiongoza kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu randama ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/26 kilichofanyika leo 24 Machi 2025



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakifuatilia kwa makini hoja zilizowasilishwa na Wizara ya Nishati wakati wa kikao cha Kamati hiyo kuhusu randama ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/26 kilichofanyika leo 24 Machi 2025

# WANANCHI NJOMBE WAIOMBA TANESCO, REA KUONGEZA KASI YA KUWAUNGANISHIA UMEME

- Hamasa ya kuunganishiwa umeme yatokana na kasi ya maendeleo katika sehemu zenye huduma ya umeme
- Kapinga asema ifikapo 2030 Wananchi wote watakuwa wamefikiwa na huduma ya umeme



Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Melela Mkoani Njombe wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakikagua maendeleo ya Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini katika vijiji vya Mkoa wa Njombe tarehe 18 Machi 2025.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Mathayo Davidi akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mtwango mkoani Njombe wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakikagua maendeleo ya Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini katika vijiji vya Mkoa wa Njombe tarehe 18 Machi, 2025.

Wananchi wa Mkoa wa Njombe ambao bado hawajafikiwa na huduma ya umeme wameiomba Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuongeza kasi ya kuwaunganishia umeme katika kaya zao ili waweze kuutumia kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Hayo yameelezwa kupitia Viongozi wa Vijiji vya Melela, Mtwango, Lwangu, Lupende na Melela wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyolenga kukagua maendeleo ya mradi wa usambazaji umeme vijijini katika vijiji vya Mkoa wa Njombe tarehe 18 Machi 2025.

Viongozi hao wamesema wananchi wameingia hamasa zaidi ya kuunganishiwa umeme baada ya kuona maendeleo yanazidi kuimarika katika baadhi ya Kaya ambazo tayari zimeunganishiwa umeme.

Aidha, wameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imetoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ukiwemo umeme katika maeneo yao ambapo kwa miaka ya hivi karibuni wamekuwa wakiona kasi kubwa ya maendeleo.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatib Kazungu akifafanua jambo kwa wananchi wa Kijiji cha Lwangu Mkoani Njombe wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakikagua maendeleo ya Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini katika vijiji vya Mkoa wa Njombe tarehe 18 Machi 2025.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga amewatoa hofu wananchi hao kwa kuwaeleza kuwa azma ya Serikali ni kuhakikisha inafikisha umeme kwa wananchi wote ifikapo 2030.

Ameeleza kuwa maendeleo katika maeneo yote hupelekwa kwa hatua kama ilivyo kwa miradi ya umeme lakini lengo la Serikali ni wananchi wote wafikiwe na huduma.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mathayo David amewasisitiza wananchi kuendelea kutandaza nyaya katika nyumba zao ili miradi ya umeme uiakapowafikia waunganishwe kwa haraka.

Ameeleza kuwa, wananchi ambao hawahitaji kusuka nyaya wafike katika ofisi za TANESCO Ili wapatiwe kifaa cha umeme tayari( UMETA) kwa gharama ya Shilingi elfu 27,000 tu.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wakala wa Nishati Vijijini(REA), Mhandisi Jones Olotu akizungumza na wananchi wa kijiji cha Lupende Mkoani Njombe wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakikagua maendeleo ya Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini katika vijiji vya Mkoa wa Njombe tarehe 18 Machi 2025.

# MHA. MRAMBA: BIASHARA YA KUUZIANA UMEME KUINUFAISHA TANZANIA

- Afafanua kuuuza na kununua umeme ni jambo la kawaida kwa nchi
- Asisitiza kununua umeme kwa Mikoa ya Kaskazini kunamanufaa kwa Mikoa husika
- Asema kukamilika kwa Mradi wa TAZA kutainufaisha Tanzania na biashara ya umeme

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba ametoa Ufafanuzi zaidi kuhusu hatua ya Serikali kununua Umeme nchini Ethiopitia kupitia Nchini Kenya hadi Namanga Mkoani Arusha utaimarisha Upatikanaji wa Umeme katika Mikoa ya Kanda ya Kaskazini ambayo kimsingi kwa sasa inatumia umeme unaozalishwa katika Mikoa ya Kusini.



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha.Felchesmi Mramba akizungumza na Waandishi wa Habari pamoja na wageni waalikwa jijini Dodoma wakati wa hafla ya kufunga rasmi Mradi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Makambako hadi Songea, uliofadhiliwa na Serikali ya Sweden na Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa Habari tarehe 10, Machi 2025 Jijini Dar es Salaam Mha. Mramba amesema ununuzi wa Umeme kutoka nchi Jirani haimaanishi kuwa nchi iko katika changamoto ya upungufu wa umeme kwa kuwa mpaka sasa Tanzania inazalisha umeme wa kutosha ambao ni Takribani Megawati 3796.

Amefafanua kuwa hatua hii ina faida kwa pande zote mbili kwa kuwa njia itakayotumiwa kununua umeme nchini Ethiopia ndio hiyo itakayotumiwa kuuza umeme kwa nchi zenye Uhitaji.

Akifafanunua zaidi amesema kuwa jinsi umeme utakavyokuwa ukinunuliwa, umeme wa Ethiopia utaingizwa kwenye mfumo wa Gridi ya Kenya na kisha Kenya itatoa umeme kuja Tanzania ikifidia umeme ulioingizwa kutoka nchini Ethiopia.

‘’Makubaliano haya yako ya pande mbili kuna wakati sisi tutanunua umeme na kuna wakati tutatumia njia hiyo hiyo kuuza umeme kwa nchi jirani, tunavyoangalia hali ya Kaskazini kwa sasa tunaona sisi tutachukua zaidi kuliko kupeleka lakini kuna wakati na wenyewe wanaweza wakahitaji umeme na tutatumia njia hiyo hiyo kuwapelekea”

Ameongeza kuwa kununua na kuuziana umeme kwa nchi si jambo geni na Tanzania kwa muda mrefu imekuwa ikinunua umeme nchini Uganda kwa ajili ya Mkoa wa Kagera, nchini Zambia kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa na nchini Kenya kwa baadhi ya maeneo ya mkoa wa Tanga hususani ya mpakani.

Aidha, amesema kuwa Tanzania inaendelea na ujenzi wa njia ya Kusafirisha umeme kutoka Tanzania Kwenda Zambia, ambapo kukamilika kwa Mradi huo kutatoa fursa kwa Tanzania kuuza umeme kwa nchi za Kusini mwa Afrika.

Kuhusu Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere ambalo mpaka sasa limefikia asilimia 99.8 kukamilika amesema limekua na mchango mkubwa wa upatikanaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

“Kule Julius Nyerere sasa hivi tunatumia umeme tunaouhitaji, kama mahitaji yetu sisi ni Megawati 1908 kwenye Gridi ya Taifa hatuwezi kuzalisha zaidi kwa kuwa umeme utakua hauna matumizi”

Pamoja na hayo Mha Mramba ameeleza kuwa Tanzania imejiunga katika masoko ya Pamoja ya kuuziana umeme ya Ukanda wa Mashariki mwa Afrika (Eastern Africa Power Pool-EAPP)

na Kusini mwa Afrika (Southern African Power Pool-SAPP) ambapo kwa upande wa Kusini mwa Afrika soko lilishaazishwa na linafanya kazi kwa nchi ambazo tayari miundombinu ilishakamilika na kwa sasa Tanzania inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa TAZA ambao kukamilika kwake kutaifanya Tanzania kutumia fursa ya umeme wa unaozalishwa kwenye Bwawa la Julius Nyerere na vyanzo vingine na kuanza kuuza umeme ukanda wa kusini mwa Africa (SAPP).

Hivyo lengo kuu la kuuza au kununua umeme ni kuimarishwa kwa mifumo ya Gridi za Umeme za nchi husika pamoja na kupunguza gharama.Kwa kuzingatia jiografia ya Tanzania itatumia nafasi ya masoko haya ya umeme kununua na kuuza umeme kutoka ukanda wa Mashariki na kusini mwa Afrika.

Serikali kupitia Wizara ya Nishati inaendelea kuhakikisha kunakuwepo na miundombinu imara itakayowezesha manunuzi na mauziano ya umeme ndani ya ukanda wa EAPP pamoja na ukanda wa SAPP ili Tanzania inufaike kwa kuuza na kununua umeme lakini pia kuingiza fedha zitokanazo na gharama za kupitishia umeme kutoka ukanda mmoja kwenda mwingine.

Wakati Miradi mbalimbali ikiendelea kutekelezwa kwa kasi kubwa, kuingiza umeme Ukanda wa Kaskazini kuna faida kubwa ikiwa ni pamoja na kuimarisha hali ya upatikanaji umeme kwenye mikoa

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI YARIDHISHWA NA HATUA ZA UTEKELEZAJI MRADI WA TAZA

- Zaidi ya Shilingi Bilioni 21 zatumika kulipa fidia waliopisha mradi
- Serikali yasema mradi utakamilika kwa wakati

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imefanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Tanzania na Zambia (TAZA) unaohusisha njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa Kilovolti 400 pamoja na Vituo 5 vya kupoza umeme kikiwamo kituo cha Kisada.Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeeleza kuridhishwa .kwake na hatua ya utekelezaji wa mradi huo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe.David Mathayo amesema hayo wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme katika Mkoa wa Iringa tarehe 19 Machi 2025 ukiwemo mradi wa TAZA.



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga akielezea mafanikio ya utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Tanzania na Zambia (TAZA) wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ikikagua miradi ya Umeme katika Mkoa wa Iringa tarehe 19 Machi 2025



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Mathayo Davidi akiongea na Wananchi wa Kijiji cha Kiseda wilayani Mafinga wakati Kamati hiyo ilipotembelea Mradi wa Umeme wa Tanzania na Zambia (TAZA) katika ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ikikagua miradi ya Umeme katika Mkoa wa Iringa tarehe 19 Machi 2025

Mhe. Mathayo amesema Mradi huo ni muhimu kwa kuwa una manufaa makubwa kwa nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika ambapo utawezesha nchi hizo kuuziana umeme kupitia Tanzania.

Ameeleza kuwa, mradi huo utakapokamilika utaimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe pamoja na kufikisha umeme wa Gridi katika Mkoa wa Rukwa.

Amesema kukamilika kwa mradi huo kutawezesha ujenzi wa njia ya kusafirisha Umeme wenye msongo wa Kilovolti 400, kutoka Sumbawanga kupitia Mpanda na ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme katika eneo la Kidahwe mkoani Kigoma hali itakayoimarisha umeme katika Mkoa wa Rukwa, Katavi, Kigoma na Tabora.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa tayari Serikali imetoa zaidi ya shilingi Bilioni 21 kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi waliopisha eneo la ujenzi wa mradi pamoja vituo vya kupoza umeme.

Kapinga amesema tayari zaidi ya shilingi Bilioni 17 zimeshalipwa kwa Wananchi zaidi ya elfu 6 ambao maeneo yao yamechukuliwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Mradi huo.

Amefafanua kuwa mradi huo unajengwa kwa fedha za Watanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Maendeleo la Ufaransa(AFD) na Umoja wa Ulaya(EU).

Akizungumzia ujenzi wa Kituo cha Kisada, Kapinga amesema zaidi ya wakazi 70 wanaozunguka eneo hilo watapata ajira za muda mfupi, huduma ya maji safi na salama pamoja na kuboreshewa Barabara ya kutoka Nyororo kwenda Kisada yenye urefu wa kilomita 15 kutoka Barabara kuu iendayo Mbeya.

Amesema Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi huo muhimu ili ukamilike kwa wakati na kuleta matokeo Chanya yaliyokusudiwa ikiwemo upatikanaji wa umeme wa uhakika na wakutosha kulingana na mahitaji ya nchi.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakikagua utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Tanzania na Zambia (TAZA) wakati wa ziara ya Kamati hiyo ikikagua miradi ya Umeme katika Mkoa wa Iringa tarehe 19 Machi 2025

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YAPONGEZA UJENZI JENGO LA WIZARA YA NISHATI MJI WA SERIKALI-MTUMBA

- Ujenzi wafikia asilimia 94

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imekagua ujenzi wa jengo la Wizara ya Nishati katika mji wa Serikali Mtumba na kuipongeza Wizara kwa hatua ya ujenzi iliyofikiwa kwa asilimia 94.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. David Mathayo amesema hayo tarehe 20 Machi 2025, wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa jengo hilo katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma iliyohusisha Menejimenti ya Wizara na baadhi ya watumishi.

"Tumepita kila mahali katika jengo hilo kazi nzuri na kubwa imefanyika na mandhari ya ndani na ya nje zote zinavutia sana, nawapongeza sana Wizara ya Nishati kwa kazi hii, zaidi kamati inampongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana za kutekeleza ujenzi wa majengo mengi na mazuri ya serikali." Amesema Mathayo

Amepongeza Viongozi Wakuu na Menejimenti ya Wizara ya Nishati kwa kusimamia vyema ujenzi huo na kuhakikisha fedha za mkandarasi zinalipwa kwa wakati wakati wote.

Aidha,amewasisitiza kukamilisha kazi ndogo zilizosalia ili watumishi waweze kuhamia katika jengo hilo mapema.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. David Mathayo akitoa maelekezo kwa kwa menejimenti ya Wizara ya Nishati wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa Jengo hilo katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma, Tarehe 20 Machi, 2025.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatib Kazungu akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kukagua ujenzi wa Jengo la Wizara ya Nishati wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa Jengo hilo katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma Tarehe 20 Machi, 2025.

Khatibu Kazungu, amesema kuwa watumishi wa Wizara ya Nishati wanatarajia kuhamia katika jengo hilo kabla ya mwezi Mei 2025 kwa kuwa kazi kubwa tayari imeshafanyika.

Dkt. Kazungu amesema watumishi wote wakihamia katika jengo kutawazesha watumishi hao kukaa sehemu moja na kufanya kazi zao kwa ufanisi tofauti na ilivyo sasa ambapo watumishi wamegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni Kikuyu na Mtumba.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakikagua ujenzi wa Jengo la Wizara ya Nishati wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa Jengo hilo katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma iliyohusisha Menejimenti ya Wizara na baadhi ya watumishi, Tarehe 20 Machi, 2025.



Muonekano wa Jengo jipya la Wizara ya Nishati linalojengwa katika mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma, Tarehe 20 Machi, 2025



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa kwenye picha ya pamoja na Menejimenti ya Wizara ya Nishati na baadhi ya watumishi wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa Jengo la Wizara hiyo linalojengwa katika mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma Tarehe 20 Machi, 2025.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatib Kazungu akiwa kwenye picha ya pamoja na Menejimenti ya Wizara ya nishati na baadhi ya watumishi wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa Jengo la Wizara hiyo linalojengwa katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma Tarehe 20 Machi, 2025.

# BILIONI 60 KULIPA FIDIA WANANCHI WALIOPITIWA MRADI WA RUHUDJI NA RUMAKALI

- Serikali ya Awamu ya Sita yapongezwa kupelekea Umeme Maeneo Korofi mwambao wa ziwa Nyasa
- Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini yaipongeza REA na TANESCO
- Zaidi ya asilimia 98 ya Vijiji vyote Njombe vina umeme

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeishauri Serikali kutafuta fedha za kuwalipa fidia wananchi waliopitiwa na Miradi ya kufua Umeme ya Ruhudji na Rumakali, ili wananchi hao wapishe maeneo hayo na waweze kuendelea na shughuli zao za kila siku wakati miradi hiyo ikisubiri kutekelezwa.

Kauli hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, ambaye ni Mbunge wa Same Magharibi Mhe. David Mathayo baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika Mkoa wa Njombe, tarehe 16 Machi 2025.

Mhe. Mathayo amesema, Serikali itafute fedha za kuwalipa fidia wananchi walioathiriwa na miradi hiyo ili wananchi hao wapishe na meneo hayo na waendelee na shughuli zao zingine wakati serikali ikiendelea kutafuta fedha za kutekeleza miradi hiyo.

" Tayari tathmini imeshafanyika kwa wananchi watakaopitiwa na mradi huo na gharama za kuwalipa zimefahamika,na wananchi wanayo hiyo taarifa, ni vyema sasa serikali ikatafuta fedha za kuwalipa fidia wananchi hao ili wakaendelee na Maisha yao mengine wakati juhudi za kutekeleza mradi hiyo zikiendelea kufanyika", alisisitiza Mhe. Mathayo.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. David Mathayo akizungumza wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika Mkoa wa Njombe, tarehe 16 Machi 2025.

Utekelezaji wa Miradi ya Ruhudji na Rumakali utaiwezesha nchi kupata zaid ya megawati 500 za umeme ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya Taifa na kuimarisha hali ya upatikanai wa umeme nchini.

Kamati hiyo imeipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupelekea umeme kwa wananchi wake kama alivyoahidi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kusema kuwa ni jambo la msingi sana kwa kuwa wananchi wamekuwa wakisubiri umeme huo kwa muda mrefu na kwa miaka mingi .

Alifafanua kuwa kuna maeneo mengine ni magumu kufikika kwa kuwa hakuna miundombinu ya Barabara na ambayo wananchi wake walikuwa hawajawahi kupata



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga, akizungumza wakati wa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika Mkoa wa Njombe, tarehe 16 Machi 2025.


Wajumbe Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakisilikza taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika Mkoa wa Njombe, tarehe 16 Machi 2025.

huduma ya umeme tangu enzi za uhuru, lakini kwa sasa wamepata umeme kutokana na umakini wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwajali wananchi wake.

Pamoja na mambo mengine amewapongeza Wakala wa Nishati Vjijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kupelekea umeme katika Vijiji na Vitongoji vya Mkoa huo ambapo katika maeneo mengine umeme huo umefikishwa kwa asilimia mia moja licha ya kuwa na miundombinu hafifu.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga, akizungumza kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, amesema Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zilizo chini yake wamepokea maelekezo ya kamati hiyo pamoja na shukrani kwa niaba ya serikali, katika kutekeleza miradi ya umeme.

Ameweka wazi kuwa shukrani hizo zinakwenda moja kwa moja kwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan,kwa kuwa ndiye amekuwa kinara katika kuhakikisha kuwa miradi ya Umeme inatekelezwa na inafahamika duniani kote kwa namna ambavyo anasimamia Nishati kwa kadri ya uwezo wake ili wananchi wengi wafikiwe na umeme.

Kuhusu suala la fidia amesema kuwa Serikali imekuwa ikilipa fidia kwa wananchi wote wanaopisha miradi mbalimbali inayoanzishwa nchini, ikiwemo hiyo ya Ruhudji na Rumakali yenye thamani ya shilingi Bilioni 63.

Akitolea mfano baadhi ya miradi ambayo wananchi wake wamelipwa fidia ni pamoja na ule ya Tanzania - Zambia (TAZA), na mradi wa kupelekea umeme wa Gridi mkoani Katavi.

Serikali ya imepanga kuhakikisha wananchi wake wanaendelea kupata umeme wa uhakika na katika Mkoa wa Njombe zaidi ya asilimia 98 ya vijiji vyote vina umeme ambapo vimebaki Vijiji tisa tu ambavyo changamoto zake zinatatuliwa ili navyo vipate umeme na kuongeza kuwa Pia wataendelea kusambaza umeme katika maeneo ya pembezoni na kuimarisha nguvu ya umeme ili wananchi wapate umeme mwingi wa kutosha kukidhi mahitaji yao.

Azma ya serikali ni kuhakikisha kuwa ikifikapo 2030 asilimia 75 ya wananchi wote nchini wawe wamepata umeme na waweze kutumia nishati safi ya kupikia.

“Kwa sasa Serikali iko hatua za mwisho katika kukamilisha mradi wa Julius Nyerere utakaozalisha Megawati 2,115, hivyo hivi karibuni it's za kutekeleza miradi ya Ruhuji na Rumkali, azma ya serikali ni kuhakikisha inaongeza vyanzo vya uzalishaji wa umeme hivyo serikali inatafuta fedha ili kuanza utekelezaji wa miradi hiyo”, alisema Kapinga.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini REA, Mhandisi Jones Olotu amesema kuwa mwambao wa Ziwa Nyasa una maeneo korofi ambayo hayafikiki kirahisi katika utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini kwa kuwa hakuna miundombinu ya Barabara na kuahidi kutafuta utaratibu maalum wa kumpata mkandarasi mahsusi wa kutekeleza kazi hiyo ambapo sasa kazi kufanya upembuzi yakinifu inaendelea .

Amesema baada kukamilika kazi ya kusambaza umeme katika maeneo hayo, itaanza na itakamilika kabla ya kufika mwezi wa Sita mwaka huu 2025 ambapo vijiji hivyo vyote vitakuwa vimewashwa Umeme.

Kwa upade Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) Renata Ndege amesema ,miradi hiyo ya Ruhuji na Rumakali itagharimu zaidi ya shilingi trilioni 4 kutekeleza miradi hiyo.

Miradi hiyo ikitekelezwa itaongeza upatikanaji wa umeme nchini pia itaboresha maendeleo ya uchumi, Ajira kwa wananchi,miundombinu ya barabara, pamoja na huduma za kijamii.

# BARAZA LA SABA LA WAFANYAKAZI WIZARA YA NISHATI LAKUTANA DODOMA

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatibu Kazungu Machi 22, 2025 amefungua Baraza la saba la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati ambalo limepitia pamoja na mambo mengine Rasimu ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kupitia hoja mbalimbali zilizowasilishwa na TUGHE.

Akifungua baraza hilo Dkt. Kazungu amesema Wizara ya Nishati itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati nchini ili kuhakikisha nchi inakua na uhakika wa upatikanaji wa nishati ya umeme, mafuta na gesi.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatibu Kazungu akizungumza wakati akifungua Baraza la saba la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati tarehe 22 Machi, 2025.

"Wizara ya nishati itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati nchini ili kuhakikisha Nchi inakuwa na uhakika wa nishati na katika kutekeleza hili wizara itahakikisha inasimamia taasisi zilizochini yake pamoja na makampuni tanzu yanayojishughulisha na nishati nchini". Amesema Dkt. Kazungu.

Kazungu ameeleza kuwa Wizara itaendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kufikisha Gridi ya taifa katika Mikoa iliyosalia ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara.

Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza mpango wa taifa wa nishati wa mwaka 2025/2026 kwa lengo la kuongeza upatikanaji na uunganishaji wa umeme kwa wananchi, kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme na mashirika binafsi katika maendeleo ya sekta ya nishati na kuhakikisha upatikanaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kutekeleza miradi wa Gridi ya taifa, kufanya matengenezo na ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme pamoja na uboreshaji njia za kusafirishaji na usambazaji wa umeme katika vitongoji, maeneo ya migodi, viwanda pamoja na vituo vya afya.

Kwa upande wa Sekta ya mafuta na gesi, Dkt. Kazungu amesema sekta ya mafuta na gesi Wizara itaendelea kuwezesha upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ,kupitia ujenzi wa vituo vya mafuta maeneo mbalimbali nchini.

Kazungu amesisitiza Wizara itaendelea kujikita katika kuwezesha utafutaji,uendelezaji na usambazaji wa gesi asilia na kutekeleza miradi ya kimkakati ya gesi asilia ikiwemo Mnazi bay Kaskazini,mradi wa kuchakata gesi asilia kuwa kimiminika (Lindi) ,utafutaji na uendelezaji na usambazaji wa mafuta ikiwemo ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Ohima (Uganda) hadi Chonholeani (Tanga-Tanzania).

Kwa upande wa nishati safi ya kupikia kwa mwaka wa 2025/2026 Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia na mpango wa Taifa wa nishati wa mwaka 2030.

Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi katika kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya nishati safi ya kupikia.

Mwenyekiti wa Balaza la Wafanya kazi Wizara ya nishati Ndugu Zuena Msuya aliweza kueleza umuhimu wa kudumisha stahiki za watumishi ili kuendeleza ufanisi wa ufanyaji kazi katika Wizara ya Nishati.

# REA YAENDELEA KUSAMBAZA MITUNGI YA GESI 19,530 MKOANI KIGOMA

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kushirikiana na kampuni ya Oryx Gas Tanzania Ltd, tarehe 14 Machi, 2025 imezindua zoezi la kusambaza mitungi ya gesi ya kilo 6 kwa wakazi wa wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma ambapo jumla ya mitungi ya gesi 3,255 itasambazwa wilayani humo kwa bei ya ruzuku ya shilingi 20,000.

Mkuu wa wilaya ya Buhigwe, Mhe. Kanali, Michael Ngayalina amezindua zoezi hilo katika Kitongoji cha Kamazi na kupongeza Serikali ya Awamu ya Sita kupitia REA pamoja na msambazaji, kampuni ya Oryx Gas kwa kuanza kugawa mitungi hiyo na kutoa wito kwa Wananchi kuchangamkia fursa hiyo ya nishati safi.

"Naipongeza REA kwa kutekeleza Mradi huu, nawapongeza Oryx Gas kwa kushirikiana na Serikali katika kusambaza nishati safi kwa Wananchi wa vijijini" amesema Mhe. Ngayalina.

Imeelezwa kuwa utekelezaji wa Mradi huo wa kusambaza mitungi ya gesi kwa mkoa wa Kigoma ulianza rasmi tarehe 3 Machi, 2025 katika wilaya ya Kasulu ambapo hadi jana zaidi ya mitungi 2,000 ilikuwa imeuzwa kwa Wananchi.

Kwa upande wake, Meneja Mradi wa Nishati Safi mkoa wa Kigoma kutoka REA; Mhandisi, Ramadhan Mganga amesema, Serikali kupitia REA imetenga fedha (Shilingi milioni 390) kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa kusambaza mitungi ya gesi (LPG) ya kilo 6 kwa mkoa wote wa Kigoma katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji; ambapo mitungi 19,530 itauzwa kwa Wananchi kwa bei ya ruzuku ya shilingi 20,000.



Mkuu wa wilaya ya Buhigwe, Mhe. Kanali, Michael Ngayalina (Kulia) akiwa na Mhandisi, Ramadhan Mganga (Kushoto) wakimkabidhi mtungi wa gesi wa kilo 6, Bi. Flora Muhitira, mwananchi kutoka kitongoji cha Kavomo kwenye Halmashauri ya wilaya ya Buhigwe baada ya kuzindua zoezi la usambazaji wa mitungi ya gesi 3,255 katika wilaya ya Buhigwe.



Mkuu wa wilaya ya Buhigwe, Mhe. Kanali, Michael Ngayalina (Kulia) akiwa na Mhandisi, Ramadhan Mganga (Kushoto) wakimkabidhi mtungi wa gesi wa kilo 6, Bwana, Kheri Kiliza mwananchi kutoka kitongoji cha Kamazi kwenye Halmashauri ya wilaya ya Buhigwe baada ya kuzindua zoezi la usambazaji wa mitungi ya gesi wilayani humo.

"Mpango huu wa kusambaza mitungi ya gesi ni mzuri na kama mnavyofahamu; Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mama Samia Suluhu Hassan aliuzindua rasmi, tarehe 27 Februari, 2025 mkoani Tanga na kutoa mwelekeo wa kuhakikisha Wananchi wanahamasishwa kutumia nishati safi, ambapo lengo hadi ifikapo mwaka 2034 angalau asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi." Amesema, Mhandisi, Mganga




Mhandisi, Ramadhan Mganga kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) akiongea katika hafla hiyo ya usambazaji wa mitungi ya gesi wilayani Buhigwe.



Wananchi kutoka kitongoji cha Kivomo wakiwa kwenye mstali wakati wa zoezi la kujiandikisha wakati wa zoezi la ununuzi wa mitungi ya gesi ya kilo 6 inayouzwa kwa bei ya ruzuku kutoka kwa msambazaji; kampuni ya Oryx wilatani Buhigwe.

"Lengo letu ni kuwawezesha Wananchi wa vijijini ili wapate nishati safi ya kupikia kwa ajili ya kupunguza athari zinazotokana na matumizi ya nishati zisizo safi. Nawaomba Wanancha wafike kwenye vituo vya kuuzia mitungi, wakiwa na Vitambulisho vya NIDA kwa ajili kununua mitungi hii pamoja na vifaa vyake kwa bei ya ruzuku ya shilingi (20,000/=) tofauti na ambavyo wangenunua kwa shilingi (56,000)". Amesisitiza Mhandisi, Mganga.

Wilaya zitakazonufaika na usambazaji wa mitungi hiyo ya gesi kwa mkoa wa Kigoma ni pamoja Kasulu, Uvinza, Kakonko, Kibondo, Kigoma na Buhigwe

# REA YAENDELEA KUTEKELEZA MKAKATI WA TAIFA WA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KWA VITENDO



Kaimu Meneja Usaidizi wa Kiufundi kwa Waendelezaji Miradi REA, Mhandisi Emanuel Yesaya akizungumza wakati wa Maonesho ya Kuelekea Siku ya Wanawake Duniani 2025 yaliyofanyika jijini Arusha tarehe 7, Machi 2025.

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) unaendelea na jitihada mbalimbali za uelimishaji, uhamasishaji na usambazaji wa bidhaa za Nishati Safi za Kupikia katika Mikoa yote Tanzania Bara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha 80% ya Wananchi wanatumia Nishati Safi za Kupikia ifikapo Mwaka 2034.

Hayo yameelezwa Machi 7, 2025 Jijini Arusha na Kaimu Meneja Usaidizi wa Kiufundi kwa Waendelezaji Miradi REA, Mhandisi Emanuel Yesaya wakati wa Maonesho ya Kuelekea Siku ya Wanawake Duniani 2025.

"Tunashiriki kutoa elimu, kuonyesha bidhaa mbalimbali za nishati safi ya kupikia na kuhamasisha wananchi hususan akina mama kutumia nishati safi ya kupikia ili kurahisisha maisha yao sambamba na kulinda afya zao," alisema Mhandisi Yesaya

Alisema REA imeandaa program mbalimbali zinazolenga kumrahisishia maisha mwanamke hasa ikizingatiwa kuwa mwanamke ndiye kinara wa jiko.

Alisema Serikali inatambua umuhimu wa kulinda afya za wananchi wake sambamba na kuhifadhi mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa yameathiriwa na matumizi ya Nishati chafu za kupikia zikiwemo kuni na mkaa na sasa mwelekeo ni kujikita katika matumizi ya Nishati Safi za Kupikia ambazo Serikali inafanya kila njia zifike kwa kila mwananchi kwa gharama anayoweza kumudu.

"Hii ni fursa adhim ambayo imetolewa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye kinara wa Nishati Safi ya Kupikia kwa wananchi wake, tunatoa rai kwa Watanzania kuchangamkia fursa hii," alisema Mhandisi Yesaya.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa REA, Bi Martha Chassama alitoa wito kwa wanawake kutembelea banda la Wizara ya Nishati ili kujifunza kwa undani umuhimu wa kutumia Nishati Safi ya Kupikia

# KAMATI YA PAC YAIPONGEZA REA USAMBAZAJI WA UMEME KATIKA VIJIJI VYA MKOA SINGIDA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) chini ya Kaimu Mwenyekiti wake, Mhe. Joseph Kakunda, tarehe 14 Machi, 2025 imetembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya kusambaza umeme vijijini mkoani Singida kupitia Miradi ya awali kama vile REA Awamu ya Kwanza (REA I), REA Awamu ya Pili (REA II), REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza (REA III Round I), na REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II); ambapo vijiji vyote 441 vya mkoa huo vimefikiwa na umeme huku vitongoji 1,052 vimefikiwa na huduma ya umeme kati ya vitongoji 2,289 vya mkoa wa Singida, sawa na asilimia 45.96 ya vitongoji vyote.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, Mhe. Kakunda ameipongeza Bodi ya Nishati Vijijini (REB); Menejimenti ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Serikali kwa ujumla kwa kubuni, kuanzisha na kutekeleza Miradi mbalimbali ya kusambaza nishati ya umeme kwa Wananchi wa mkoa wa Singida na kuongeza kuwa umeme ni fursa ya kuboresha maisha ya Watu vijijini kama utatumika ipasavyo.

"Tumefurahishwa na tuliyoyaona hapa katika kijiji cha Kitopeni; Aghondi na kwenye zahanati ya kijiji cha Mabondeni. Tunaishukuru Serikali kupitia REA kwa udhibitisho wa uwepo wa umeme. Tunatoa wito kwa Wananchi, kasi ya kujiunganisha na huduma ya umeme, iongezeke; wekeni mpango ili kuhakikisha umeme unawasaidia kujiletea maendeleo yenu." Amesema, Makamu Mwenyekiti wa PAC, Mhe. Kakunda.



Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB); Mhe. Balozi na Meja Jenarali Mstaafu, Jacob Kingu (Mwenye kofia) akitoa maelezo mafupi wakati akijibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe Kamati ya PAC walipotembelae Miradi inayotekelezwa na REA katika mkoa wa Singida.




Katibu Tawala wa mkoa wa Singida, Dkt. Fatuma Mganga (Wa kwanza kushoto) akiwahamasisha Wananchi wa kijiji cha Aghondi kuhusu kuchangamkia fursa za uwepo wa umeme vijijni kwa ajili ya kuutumia kama nyenzo ya kujikwamua kiuchumi.

Katika taarifa yake mbele ya Kamati ya PAC; Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti Bwana Godfrey Chibulunje ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa REA; amesema Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imetoa jumla ya shilingi bilioni 86.8 ili kuhakikisha Miradi minne (4) inatekelezwa mkoani humo ili kuhakikisha Wananchi wanafikiwa na huduma ya umeme ili kuwapa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Wakala wa Nishati Vijijni (REA) unaendelea kutekeleza miradi mbalimbali pamoja na kuwasimamia kwa karibu wakandarasi wote waliopewa zabuni ya kutekeleza miradi mbalimbali kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliopangwa ili iweze kuwanufaisha Wananchi."amesema Bwana Godfrey Chibulunje.



Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) Mhe. Joseph Kakunda, akizungumza na Wananchi wa kijiji cha Aghondi katika Halmashauri ya wilaya ya Manyoni mkoani Singida wakati Wajumbe wa Kamati hiyo wakati za ziara hiyo.



Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe Kamati ya PAC wakiwa nje ya Mradi wa mashine ya kuongeza thamani mazao ya kilimo (Mashine ya kusaga na kukoboa nafaka) katika kijiji cha Aghondi Halmashauri ya Manyoni wakati wa ziara ya Kamati hiyo.



Mradi wa mashine ya kuongeza thamani mazao (Mashine ya kusaga na kukoboa nafaka); Mradi unaomilikiwa na Mwananchi wa kijiji cha Aghondi Bwana Adam Mwandi (Hayupo pichani).



Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe Kamati ya PAC wakielekea kwenye zahanati ya kijiji cha Mabondeni; zahanati ambayo iliunganishwa na huduma ya umeme ambapo umeme unatumika kuhifdhi chanjo mbalimbali pamoja na kutoa huduma hadi nyakati za usiku kutokana na upatikanaji wa nishati hiyo.